NYIMBO ZA BIBLIA

	KUJENI (Venite)	p 18
	MUBARIKI (Te Deum)	p 19
	MUFURAHI (Jubilate)	p 20
	MUMUSIFU (Benedicite)	p 21
	UTUKUFU (Gloria)	p 22, 48
Wimbo wa	MARIA (Magnificat)	p 22, 23, 24
Wimbo wa	ROHO MUTAKATIFU	p 25
Wimbo wa	SIMIONI (Nunc Dimmitis)	p 25
Wimbo wa	UFUFUKO	p 26, 27
Wimbo wa	ZEKARIA (Benedictus)	p 27
Wimbo wa	JIONI	p 28

KUJENI (Venite) - Zaburi 95:1-7, 96:13

1. Kujeni tuimbie Bwana:
   Tufanye shangwe kwa mwamba wa wokovu wetu.
2. Tuje mbele yake kwa asante:
   Tumufanyie shangwe kwa zaburi.
3. Kwa kuwa Bwana ni Mungu mukubwa:
   Na Mufalme mukubwa juu ya miungu yote.
4. Mabonde yote ya inchi ni mukononi mwake:
   Pahali pa juu pa milima ni pake vilevile.
5. Bahari ni yake naye aliifanya:
   Na mikono yake ilifanya inchi kavu.
6. Kujeni tuabudu na kuinama:
   Tupige magoti mbele ya Bwana mwenye kutuumba.
7. Kwa maana yeye ndiye Mungu wetu:
   Nasi ni watu wa malisho yake, na kondoo za mukono wake.
8. Leo, Ee kama mungesikia sauti yake:
   Kwa maana anakuja kuhukumu inchi.
9. Atahukumu ulimwengu kwa haki,
   Na mataifa kwa kweli yake.

   Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
   kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa,
   hata milele na milele. Amina.

MUBARIKI (Te Deum)

1. Ee Mungu, tunakusifu:
   tunakuamini wewe ndiwe Bwana.
2. Ulimwengu wote wanakuabudu: Ee Baba wa milele.
3. Malaika zote wanakupazia sauti:
   Nazo mbingu na nguvu zote zilizomo.
4. Makerubi na Maserafi: wanakuimbia daima.

5. Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu:
   Bwana Mungu wa uwezo na mamlaka.
6. Mbingu na inchi zimejaa: heshima ya utukufu wako.
7. Kundi tukufu la mitume: wanakusifu.
8. Kundi tukufu la manabii: wanakusifu.
9. Jeshi tukufu la washuhuda: wanakusifu.
10. Kanisa takatifu po pote: wanakuamini.
11. Baba Mungu: wa heshima kuu.
12. Tena Mwana wako pekee: wa kweli wa kuabudiwa.
13. Na Roho Mutakatifu: Musaidizi.
14. Ee Kristo ndiwe Mufalme wa utukufu:
    Ndiwe Mwana wa milele wa Baba.
15. Ulipochukua muzigo wa kuokoa watu:
    Hukuchukia tumbo la Bikira.

16. Uliposhinda uchungu wa kufa:
    uliwafunulia waamini wote ufalme wa mbinguni.
17. Umekaa mukono wa kuume wa Mungu:
    Katika utukufu wake Baba.
18. Tunaamini kwamba utakuja: kuwa Muhukumu wetu.
19. Kwa hivyo, tunakuomba uwasaidie watumishi wako:
    Uliowakomboa kwa damu yako ya damani.
20. Wahesabiwe pamoja na watakatifu wako:
    Katika utukufu wa milele.
21. Uwaokoe watu wako: uubariki uriti wako.
22. Uwatawale uwainue: hata makao ya milele.
23. Tunakutukuza kila siku:
    tunalisifu jina lako sasa, hata milele.
24. Ukubali Ee Bwana: kutulinda leo tusitende zambi.
25. Utuhurumie, Ee Bwana utuhurumie.
26. Utuonee huruma, Ee Bwana:
    kwa vile tulivyokutumaini wewe.
27. Nimekutumaini wewe Bwana:
    nisiharibike milele. **Amina.**

MUFURAHI (Jubilate) - Zaburi 100

1. Mufanyie Bwana shangwe,
   Ninyi inchi zote.
2. Tumikieni Bwana kwa furaha;
   Kujeni mbele yake kwa kuimba.
3. Mujue kwamba Bwana ni Mungu:
   Ni yeye aliyetuumba, na sisi ni wake;
   Sisi ni watu wake, na kondoo za malisho yake.

4. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru,
   Na katika viwanja vyake kwa sifa:
   Mumushukuru, na kubariki jina lake.
5. Kwa kuwa Bwana ni mwema;
   Rehema yake ni ya milele;
   Na uaminifu wake vizazi na vizazi.
   Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
   Kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa,
   Hata milele na milele. Amina.

MUMUSIFU (Benedicite)

1. Ninyi kazi zote za Bwana, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
2. Ninyi malaika za Bwana, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
3. Ninyi wana wote wa watu, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
4. Ninyi watu wa Mungu, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
5. Ninyi makasisi ya Bwana, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
6. Ninyi watumishi wa Bwana, mubariki Bwana:
   Mumusifu, mumutukuze milele.
7. Tumubariki Baba na Mwana na Roho Mutakatifu:
   Tumusifu, tumutukuze milele.
8. Ubarikiwe, Ee Bwana, katika anga ya juu:
   Kusifiwa na kutukuzwa, juu ya vyote milele. **Amina.**

UTUKUFU (Gloria in excelsis)

KUIMBWA *(kusemwa ni kwa Ushirika Mutakatifu, ukurasa 48)*

Utukufu!
Utukufu kwa Mungu juu mbinguni
Na salama duniani (x2)

1 Tunakusifu, tunakubariki, tunakuabudu utukuzwe;
Tunakushukuru kwa ajili ya utukufu wako mukuu.
Bwana Mungu, mufalme wa mbinguni Mungu Baba mwenyezi.

2 Ee Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo uturehemu.
Ee Bwana Mungu Baba, Mwana-kondoo uturehemu.
Mwana wa Baba, unayeondoa zambi za dunia uturehemu.

3 Unayeondoa zambi za dunia, upokee ombi letu.
Unayekaa kwa Mungu Baba, Baba wetu, uturehemu.

4 Kwa maana wewe peke yako Bwana,
wewe peke yako Mutakatifu,
wewe peke yako Kristo, na Roho Mutakatifu,

uliye juu, uturehemu! Kwa utukufu,
kwa Mungu Baba, tunakusifu, Amina.

|s :s :l :s |
s,:s,.s,:-.s,:s,	d:d:- :-	m:-.d:r:d	l,:-:
f :-.r:m:d	t,:-:d:r	d :-:
s,:s,:s,:s,	d:-:d :-	m :-.d:r:l,	r :-:
f :-.r:m:d	t,:-:d:r	d :-:

Wimbo wa MARIA (Magnificat) - Luka 1:46-55

A.

1 Moyo wangu unamusifu Bwana:
na roho yangu inamufurahia Mungu, Mwokozi wangu.

2 Kwa maana amenikumbuka mimi mutumishi wake
munyenyekevu:
tangu sasa watu wote wataniita mwenye heri.

3 Kwa sababu Mungu mwenye uwezo amenitendea matendo makubwa:
jina lake ni takatifu.

4 Huruma yake inadumu juu ya wale wanaomwogopa:
kizazi hata kizazi.

5 Ametenda mambo makubwa kwa uwezo wa mukono wake;
amewasambaza wanaojivuna katika mioyo yao.

6 Amewashusha wenye vyeo kutoka katika viti vyao:
lakini amepandisha wanyenyekevu.

7 Ameshibisha wenye njaa na vitu vyema:
na wenye mali amewaondosha mikono mitupu.

8 Amemusaidia mutumishi wake Israeli:
akikumbuka kuonyesha rehema yake.

9 Kwa Abrahamu na uzao wake hata milele:
kama alivyowaahidia baba zetu.
Utukufu...

B. KUIMBWA:

Sifu, sifu Mungu, Ee moyo wangu, usifu Mungu!
Furahi, roho yangu, na baraka zake Bwana!

1 Mimi, mutumishi, nimekumbukwa, na Mwokozi;
milele watu wote wataniita mwenye heri.
Bwana, Bwana wetu, anapandisha wanyenyekevu;
lakini anashusha watawala toka kwao.

2 Mukono wake Bwana una uwezo mukubwa sana;
Tusifu jina lake, takatifu kwa milele.
Watu, wenye mali, wanarudishwa pasipo kitu.
Wengine, masikini, wanashiba, na vitu vyema;

3 Watu wa Israeli wamepokea usaidizi;
Uzao wa Abrahamu wameona neema yake.
Sasa, sasa hivi, ametimiza ahadi zake:
Vizazi na vizazi, watapasha neno lake.

Sifu, Mungu Baba, sifu Mwana, naye Roho;
Wote ni mumoja, leo, kesho na milele.

|m :d•-:-|m:r•f:r|r:r.d•r.t,:-|r:r.d•m.d:-|
|m.m:d•-:-|m:r•f:r|r:-.d•r.t,:-|r:-.d•m.d:-|

C. KUIMBWA

Maria akasema: Moyo wangu unasifu Bwana. Unasifu!
Maria akasema: Moyo wangu unasifu Bwana.

Roho yangu imefurahia ' Mungu mwenyezi wangu.
Ametazama unyenyekevu ' wa mujakazi wake.

Tangu sasa watu wote, ' wataniita heri.
Maana amenitendea ' mambo makubwa tele!

Mungu amesambaza ' wenye majivuno,
katika mafikiri ' ya mioyo yao.

Ameshusha wakubwa ' katika viti vyao.
Amepandisha wanyenyekevu, ' kwa mukono wake.

Ameshibisha wenye njaa ' na vitu vyema.
Ameondosha wenye mali ' mikono mitupu.

Amesaidia mutumishi ' wake Israeli.
Kama alivyosema ' kwa baba Abrahamu.

|d.m:-.d•m:s|f.f:f.f•s:l|s.s:-.f•m:r|d:s.s•l:s|
|d.m:-.d•m:s|f.f:f.f•s:l|s.s:-.f•m:r|d:-•-:

:s|s:f•m:r|d:d•-:s|s:m•d:m|r:r•-:
:s|s:f•m:r|d:d•-:s|s:m•d:m|r:r•-:-|

Wimbo wa ROHO MUTAKATIFU

- Mdo 1:8, Mdo 2, Yn 16, Gal 5:22, 1 Kor 12

1 Mwokozi aliahidi wanafunzi wake atawatumia
Roho yake toka mbingu, kuwasaidia pahali pote

Matunda ya Roho huyu:
Ni neema, mapendo, salama, furaha.

2 Roho huyu kwa Pentekote akawafikia, na moto toka juu:
wakahubiri, wakabatiza, wakaponyesha watu wengi.

3 Roho moja anagawia kila mukristo zawadi nyingine:
kutabiri, au kufundisha, hata kufanya maajabu.

4 Wakristo tukiamini atatutumia Roho wa uwezo,
Musaidizi hata milele, watu wengine waokoke.

s,:- :m	d:-:m	r:m:f	f:-:f	f:s:f	m:d:-.m	f.m:r:r	t,:-
s,:s,:m	d:-:m	r:m:f	f:-:f	s:f:m	d:m:t,	r :-:d	- :-
s,:d :d	l,:l,:l,	d:s,:-
d :m:-	d :- :d	m:-:r	-:m:f	l,:s,:-	t,:r:-:d

Wimbo wa SIMIONI (Nunc Dimittis) - Luka 2:29-32

A.

1 Sasa, Bwana, kwa vile ahadi yako imetimizwa:
unaweza kumuruhusu mutumishi wako afe katika salama.

2 Kwa maana macho yangu yameona wokovu wako:
ulioweka tayari mbele ya watu wote.

3 Ni nuru itakayojulisha njia yako kwa mataifa:
na kuleta utukufu kwa watu wako Israeli.
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:
Kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa,
Hata milele na milele. Amina.

B. KUIMBWA

1 Tushukuru Bwana Mungu anayetimiza
neno aliloahidi: kutuokoa.
Bwana, sasa uruhusu sisi tupumzike.
Macho yetu yameona wokovu wako.

2 Bwana umetuma nuru kwa kila taifa
Watu wote wanaweza kutubu zambi.
Nuru inatujulisha njia yako safi;
inaleta utukufu kwa Israeli.

3 Utukufu kwa Utatu: Baba, Mwana, Roho;
Usifiwe tangu sasa na kwa milele.
Bwana, sasa uruhusu sisi tupumzike.
Macho yetu yameona wokovu wako.

|m :-.r•d.r :m.f|s:-•m:-|m:m•r:d|r:-•r:-|
|m :-.r•d.r :m.f|s:-•m:-|m:-•f:r|d:-•d:-|

|s :-.s•l.d':t.l|s:-•m:-|m:m•r:d|r:-•r:-|
|s :- •l.d':t.l|s:-•m:-|m:-•f:r|d:-•d:-|

Wimbo wa UFUFUKO 1 Kor 5:7-8 Rom 6:9-11 1 Kor 15:20-23

A. KUSEMWA AU KUIMBWA:

1. Kristo, Pasaka yetu amekwisha kutolewa kwa ajili yetu:
   basi tufanye karamu,
2. Si kwa chachu ya zamani, wala kwa chachu ya uovu na ubaya:
   lakini kwa mukate usiochachwa, ndio moyo safi na kweli.
3. Kristo akikwisha kufufuka toka wafu, hakufi tena;
   wala kufa hakumutawala tena.
4. Kwa kule kufa kwake, alikufia zambi mara moja:
   lakini kwa kule kuishi kwake, anaishi kwa Mungu.
5. Hivyo ninyi mujihesabu wenyewe kuwa wafu kwa zambi;
   lakini walio hai kwa Mungu katika Yesu Kristo Bwana wetu.
6. Lakini sasa Kristo amefufuliwa toka wafu:
   malimbuko yao waliolala.
7. Maana kwa kuwa kufa kuliletwa na mutu:
   hivyo ufufuko wa wafu uliletwa na mutu.
8. Kwa sababu kama katika Adamu wote wanakufa:
   hivyo wote katika Kristo watapatizwa uhai.
   Utukufu kwa Baba...

B. KUIMBWA:

1 Yesu Kristo, Mwana Kondoo, ni Pasaka yetu
Amekwisha kutolewa kwa ajili yetu.
Aleluya, aleluya, amefufuka, hakufi tena
Malimbuko toka wafu: tutaishi pia.

2 Si kwa chachu ya zamani, wala chachu mbaya,
Mukate usiochachwa, moyo wa ukweli.

3 Alikufa, mara moja kuondoa zambi.
Sisi tuwe wafu naye, tufufuke wahai!

4 Vile kufa kuliletwa na mutu mumoja,
Vile uhai uliletwa na Yesu Kristo tu.
Aleluya, aleluya, tunatukuza Mungu Mwenyezi:
Baba, Mwana, naye Roho, milele, Amina.

d.d:m.s: -	l.f:l.s:-	s.f:m.r:-	m.d:-:-.
d.d:m.s: -	l.f:l.s:-	s.f:m.r:-	m.d:-:-.
d'.d':d'.d':-	l.f:l.s:-
d'.r':d'.t :t.l	s.s:f.m:-
d.d:m.s: -	l.f:l.s:-	s.f:m.r:-	m.d:-:-.

Wimbo wa ZEKARIA (Benedictus) - Luka 1:68-79

1. Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli:
   Kwani amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa.
2. Ametunyanyulia pembe ya wokovu:
   Katika nyumba ya mutumishi wake Daudi.
3. Kama alivyosema kwa vinywa vya manabii yake
   watakatifu:
   Waliokuwa tangu mwanzo.

4. Tuokolewe toka adui zetu:
   Na katika mikono ya wote wanaotuchukia.
5. Kuwatendea rehema baba zetu:
   Na kukumbuka agano lake takatifu.
6. Kiapo alichomwapia Abrahamu baba yetu:
   Ya kwamba atatupa sisi,
7. Tukiokolewa toka mikono ya adui zetu:
   Tumwabudu pasipo woga.
8. Katika utakatifu na katika haki mbele yake:
   Siku zote za maisha yetu.
9. Nawe, Mutoto, utaitwa nabii lake Mungu aliye juu:
   Kwa maana utatangulia mbele ya uso wake Bwana,
   Kutengeneza njia zake.
10. Kujulisha watu wake wokovu:
    Katika kusamehewa zambi zao.
11. Kwa sababu ya upole wa rehema zake Mungu wetu:
    Katika mwanga uliotoka juu kutufikia.
12. Kuwaangazia wanaokaa katika giza, na katika kivuli cha mauti:
    Na kuongoza miguu yetu katika njia ya salama.
    Utukufu kwa Baba...

Wimbo wa JIONI (Te lucis)

1 Mwishoni mwa muchana huu, tunakuomba ee Mungu:
  Utuzungushe kila saa, na malaika za furaha.
2 Ndoto za uovu pinga, na shaka ya usiku zima:
  Mawazo yetu utakase, adui yetu ufukuze.
3 Tunakusihi Ee Baba, kwa jina la Yesu Mwana:
  Katika Roho aliye pumuzi ya uhai tele. Amina.

:r:f:f:f:f :s:f:m:-:r:r:r:r:m:m:r:d:-:
:m:m:r:d:l,:d:r:r:-:f:f:f:m:r:m:r:d:-:
d:r:d:-:d:-: